

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA MAKAMU WA RAIS**



TAARIFA KWA UMMA KUHUSU UKIUKWAIJI WA MATAKWA YA SHERIA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA NA KANUNI ZAKE WAKATI WA KUSAFIRISHA NJE YA NCHI AINA MBALIMBALI YA CHUMA CHAKAVU

Ndugu Wanahabari,

Kwa mujibu wa Sheria ya Usimamizi wa Mazingira, Sura ya 191 na Kanuni zake, Ofisi ya Makamu wa Rais imepewa Mamlaka ya kusimamia na kuratibu masuala yote yanayohusu Mazingira nchini. Aidha, Kifungu cha 133(1) na (3) cha Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 pamoja na Kanuni za Usimamizi na Udhibiti wa Taka Hatarishi za Mwaka 2021, zinampa Mamlaka Waziri mwenye dhamana ya Mazingira kutoa vibali vya kukusanya, kuhifadhi, kusafirisha ndani ya nchi, kuingiza nchini, kusafirisha nje ya nchi na kuitisha nchini taka hatarishi.

Taka hatarishi au taka zenyе madhara ni pamoja na vyuma chakavu, taka za kieletroniki, dutu hatarishi, mafuta machafu, matairi chakavu, taka za plastiki, taka zitokanazo na huduma za kitabibu, betri zilizotumika na aina ya taka zote zinazotoka migodini. Taka hizi hatarishi zinaweza kusabisha athari kwa afya ya binadamu, viumbe hai na mazingira. Ili kuzuia na kudhibiti athari hizo zitokanazo na taka zenyе madhara, mfumo mahsusii unaofanya kazi kwa ufanisi wa kudhibiti taka hizi unapaswa ufuatwe kama ulivyobainishwa kwenye Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 na Kanuni zake.

Ndugu Wanahabari,

Katika kipindi cha hivi karibuni, kumekuwepo na taarifa za usafirishaji wa aina mbalimbali ya chuma chakavu ikiwemo chuma dongo (*Cast Iron*) nje ya nchi. Hata hivyo, katika kipindi cha mwezi Machi hadi Septemba, 2023, Ofisi ya Makamu wa Rais kupitia Waziri mwenye Dhamana ya Mazingira, haijatoa kibali cha kusafirisha chuma dongo wala shaba nje ya nchi.

Hivyo, ni dhahiri kuwa kuna baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu ambao wanakiuka matakwa ya Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 na Kanuni zake kwa kusafirisha nje ya nchi chuma chakavu vyatia aina mbalimbali vikiwemo chuma dongo bila ya kuwa na vibali vinavyotolewa na Waziri mwenye dhamana ya Mazingira.

Ikumbukwe kuwa, kupitia usafirishaji wa taka hatarishi nje ya nchi, zipo tozo, ada na kodi zinazopaswa kulipwa, hivyo usafarishaji wa taka hizo bila kibali husababisha Serikali kukosa mapato yanayopaswa kulipwa kupitia usafirishaji huo. Ikumbukwe kwamba serikali kupitia TRA imeweka tozo husika kwa mujibu wa sharia, hivyo kitendo cha utoroshaji wa aina yejote kinaikosesha serikali mapato sambamba na kuwepo na uwezekano wa uharibifu wa miundombinu kutokana na kutofuatwa kwa sharia na miongozo ya serkali iliyopo. Suala la usafirishaji wa aina yejote ya chuma chakavu nje ya nchi bila ya kuwa na vibali ni uvunjaji wa sheria za nchi.

Vilevile, ikumbukwe kwamba Serikali ya awamu ya sita imeweka mkazo mkubwa katika suala la uwekezaji wa viwanda vyatia ndani kwa lengo la kuzalisha ajira na kukuza uchumi. Usafirishaji wa bidhaa mbalimbali za chuma chakavu ikiwemo chuma dongo (Caste Iron) nje ya nchi kiholela na usiofuata utaratibu unaweza kusababisha upungufu wa malighafi kwenye viwanda vinavyotumia malighafi za aina hiyo hapa nchini kwaajili ya uzalishaji wa bidhaa mbalimbali zikiwemo nondo na bomba za chuma. Upungufu wa malighafi unaweza kusababisha kupungua kwa ajira kwa vijana wanaofanyakazi katika viwanda vyetu vyatia ndani pamoja na kupanda kwa bei za bidhaa aina ya nondo na bomba za chuma ambazo zinatumika sana katika shughuli za ujezi wa nyumba za wananchi, ujenzi wa majengo ya serikali na sekta binafsi, pamoja na ujenzi wa wamiundombinu mbalimbali ikiwemo barabara, reli, madaraja, na mabwawa ya kuzalisha umeme.

Ndugu Wanahabari,

Sheria ya Usimamizi wa Mazingira Sura ya 191 Kifungu cha 13 (3) na (4) inampa Waziri mwenye Dhamana ya Mazingira, Mamlaka ya kutoa maelekezo kwa Taasisi za Serikali kufanya na kutofanya jambo lolote ambalo kwa matokeo yake mazingira yanaweza kuathiriwa.

Kwa muktadha huo, ninazielekeza Mamlaka za udhibiti zilizopo kwenye maeneo ya mipaka mbalimbali nchini kuhakikisha kwamba shehena yoyote ya taka hatarishi ikiwemo chuma dongo inayosafirishwa nje ya nchi yetu, inafuata masharti ya Kanuni za Udhibiti na Usimamizi wa Taka Hatarishi za Mwaka, 2021 ikiwemo kuwa na kibali kilichotolewa na Waziri mwenye dhamana ya Mazingira. Naielekeza **NEMC** kusimamia na kushirikiana na vyombo na Mamlaka zote za udhibiti zilizopo mipakani katika utekelezaji wa maelekezo haya.

Mwisho,

Natoa rai kwa wananchi na wafanyabiashara wanaojihusisha na biashara ya taka hatarishi hapa nchini kuzingatia matakwa ya sheria ya Mazingira na Kanuni zake. Tahadhari inatolewa kwa yeote anayejishughulisha na shughuli za kukusanya, kuhifadhi, kusafirisha ndani ya nchi, kuingiza nchini, kusafirisha nje ya nchi na kupitisha nchini taka hatarishi bila kibali, atakuwa ametenda kosa la kisheria na attachukuliwa hatua kwa mujibu wa sheria..

Asanteni kwa kunisikiliza.

Mhe. Dkt. Selemani Saidi Jafo (Mb.)

Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Rais – Muungano na Mazingira

21 SEPTEMBER, 2023